

Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 01 Issue: 01 | June-2022

EAJK

# Mikakati ya Usemi Inayodhihirisha Uanaharakati wa Kijamii katika Muziki wa Genge Nchini Kenya

**Authors**
**Lucy W. Mugo[(1)]; Florence Mwithi[(2)]; Gwachi Mayaka[(3)]**
**Main author email:** Lucym2037@gmail.com

(1.2.3) Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya.

Cite this article in APA
Mugo, L. W., Mwithi, F., & Mayaka, G. (2022). Mikakati ya usemi inayodhihirisha uanaharakati wa kijamii katika muziki wa genge nchini Kenya. *Eastern Africa journal of Kiswahili, 1*(1), 6-15. https://doi.org/10.51317/eajk.v4i1.48

OPEN ACCESS
A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 11.04.2022
Accepted: 13.05.2022
Published: 30.06.2022

**Scan this QR to read the paper online**

**Copyright**: ©2022 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

**Ikisiri**
Makala haya yanahakiki mikakati ya usemi inayotumika kudhihirisha maudhui ya uanaharakati wa kijamii katika Muziki wa Genge. Muziki wa Genge ni mojawapo wa aina ya muziki nchini Kenya ambao unapendwa sana na vijana. Muziki huu ni jambo lisiloweza kupuuzwa kwani ni sauti ya vijana. Mintaarafu ya hayo, makala haya yalihakiki matini ya Muziki wa Genge kama jukwaa la uanaharakati wa kijamii. Mikakati ya usemi ina uhusiano mkubwa na maudhui kwani humwezesha msanii kuwasilisha maudhui. Mtazamo wa Norman Fairclough katika nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi uliongoza utafiti huu. Muundo wa utafiti huu ni wa kiuthamano na kimaelezo na ulifanyika maktabani. Mtafiti alitumia sampuli kusudio kuteua nyimbo tano za Genge zifuatazo: *Kuna Siku Youth Wataungana* ulioimbwa na Wakadinali, *Kwenda* ulioimbwa na Khaligraph Jones, *Khalicartel 3* ulioimbwa na Khaligraph Jones, *Tujiangalie* ulioimbwa na Sauti Sol na *Wajinga Nyinyi* uliimbwa na King Kaka. Ukusanyaji wa data ulihusisha kusikiliza na kutazama nyimbo hizo katika mtandao wa You tube. Matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kutoa mwanga kuhusu maswala yanayowakumba vijana. Aidha matokeo haya yatakuwa malighafi katika taaluma za isimu na fasihi pamoja na uchanganuzi diskosi matini.

**Maneno muhimu:** Mikakati ya usemi, uanaharakati wa kijamii, vijana, muziki wa genge.

**UTANGULIZI**

Nyimbo za uanaharakati wa kijamii ni mojawapo ya vipera muhimu vya nyimbo (Finnegan 1970; Wamitila 2003). Mbali na kuwavutia binadamu na kuteka nadhari yao, nyimbo hizi hufumbata uhalisia wa yale wanayoyapitia wanajamii. Humwezesha msanii kuufumbata upana na urefu wa hali halisi ya maisha katika maneno teule machache yaliyofinyangwa kisanaa. Hii ni kwa sababu masuala mengi ya jamii huendeshwa kwa misingi ya uanaharakati na hivyo nyimbo za uanaharakati wa kijamii hazikosi mchango wake katika kutoa mwongozo wa kijamii. Nyimbo za uanaharakati wa kijamii zina historia ndefu katika jamii. Zimetumika kuhamasisha wanajamii kuhusu maswala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Ngugi (2000) anaelezea kuwa muziki sio wazo la dhana fulani tu bali ni tukio ambalo huwasilisha mambo mbalimbali yaliyo muhimu katika jamii. Kutokana na hayo, muziki basi ni zaidi ya sauti tu ambazo huimbwa na kuchezwa. Huwa nguzo maalum za kushamirisha suala la uanaharakati wa kijamii. Huweza kutumika kama sauti na satua ya kuleta mabadiliko katika jamii. Hivyo basi, Muziki wa Genge unakuwa nyenzo maarufu sana kwa vijana ya kushamirisha uanaharakati wa kijamii na ni jambo lisiloweza kupuuzwa kwani ni sauti ya vijana.

Kwa mujibu wa Ntarangwi (2009), muziki ni matini inayatokana na mtagusano wa jamii. Matini yoyote ile ni mali ya jamii na matini hiyo itatekeleza wajibu wake kutegemea matarajio ya jamii ambamo matini hiyo imezalishwa. Kwa hivyo nyimbo zote ni zao la jamii na ni njia mojawapo ya kupitisha ujumbe kwa wasikilizaji kwa kuangazia maswala yote kuhusu jamii. Muziki wa Genge ni aina ya muziki wa kizazi kipya wa kufoka au *kurap* na kughani unaopendwa na kusikilizwa na idadi kubwa ya vijana nchini Kenya (Wasike, 2011; Kidula, 2012). Huhusisha midundo miepesi ya ngoma na ya kasi zaidi. Mbali na hayo, huwasilishwa kwa mtindo wa kidayalojia unaoufanya wimbo uwe kana kwamba ni maongezi ya kawaida kati ya msanii na hadhira yake. Husheheni mistari ambayo ni rahisi kukumbukika. Huwa na mkarara ambao hujitokeza kama sehemu ya majibizano kati ya msanii na hadhira. Muziki huu hutumia upekee wa mtindo wake ambao mbali na kufokafoka na kughani hutumia mafumbo, jazanda, semi pamoja na matumizi ya lugha ya sheng. Muziki huu kwa sasa ni miongoni mwa nyenzo muhimu ya kuhodhi ukubalifu katika jamii ambayo inatumiwa na vijana katika kuzungumzia masuala mbalimbali yanayoihusu jamii yao.

Dhana ya uanaharakati wa kijamii inaweza kufafanuliwa kama juhudi za kuwazindua watu kutokana na hali zinazowazuia kuishi maisha yenye ufanisi. Kiongera (2010) anahoji kuwa uanaharakati wa kijamii ni jitihada za kuleta mageuzi katika jamii na kwamba vijana wanaweza kutumika kuleta mageuzi haya. Udhaifu mwingi umejitokeza katika uongozi ukijumuisha unyanyasaji, matumizi mabaya ya mamlaka, ubinafsi na uendelezaji wa ubaguzi wa vijana miongoni mwa mambo mengine. Kwa upande mwingine ukosefu wa ajira, kazi zenye ujira duni, rushwa, miundombinu duni, huduma duni za kiafya na mengineyo mengi huwafanya vijana kuumia zaidi.

Katiba ya Kenya (2010) inaelezea kijana kama mtu wa jinsia ya kiume au ya kike aliye na umri wa kati ya miaka 15 na 35. Matokeo ya Sensa yaliyotolewa na KNBS 2022, yanaonyesha kuwa vijana ni asilimia 72.4, hali hii huwafanya vijana kuwa kiungo muhimu cha jamii na taifa kwa jumla; ni nguvu na ishara ya ufanisi wa jamii yoyote. Wana nafasi muhimu katika jamii za Kiafrika kiuchumi, kisiasa na kijamii. Koster (2013) anadai kuwa nchini Kenya kumekuwa na lalama kwamba vijana hawashirikishwi katika maswala ya kisiasa, uchumi, kielimu na kijamii. Jamii imeundwa kwa namna kwamba watu walio na uwezo wanawanyima haki vijana. Hali hii husababisha migogoro na kuathiri mawasiliano kati ya vijana na wanajamii wengine. Suala ambalo baadhi ya wanajamii hulikubali na kulichukulia kama la kawaida. Mintaraafu ya haya, vijana wamezuka na mikakati mbalimbali ya kuasi ukubalifu na ukawaida huu. Muziki wa Genge ni mojawapo ya chombo maalum kinachotumika na vijana kuangazia matatizo yanayowakumba katika jamii. Muziki huu huimbwa na vijana na unahusu matini zinazowahusu, na ambazo huhusu vijana wenzao.

Makala haya yanaangazia mikakati ya usemi ambayo hutumiwa na wasanii wa Muziki wa Genge kuwasilisha ujumbe wao wa kiharakati. Leech (1969) anafafanua mikakati ya usemi kama jinsi lugha inavyotumiwa katika matini. Anaendelea kuelezea kuwa matini yoyote ile huathiriwa kwa kiasi kikubwa na mikakati ya usemi ambayo imetumika kwa sababu katika kila muktadha msemaji huchagua jinsi ya kuzungumza. Nkumbo (2019) anaelezea kuwa mikakati ya usemi

hujaribu kujibu swali la ni vipi? Hivyo basi, ubunifu wa mtunzi na uwezo wake wa kuteua mikakati ya usemi mwafaka ndivyo vifaa vinavyomwezesha kuwasilisha maudhui yake. Chepkorir (2016) anahoji kuwa mikakati ya usemi hufanya wimbo uwe wa kuvutia na wenye mnato pamoja na kusisitiza ujumbe unaowasilishwa. Huiteka nadhari ya hadhira na kuifanya ifikirie, ijisaili na kujisakura.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Nyimbo hupima uzuri wake kwa kuzingatia mikakati ya usemi inayotumika kupitisha ujumbe kwa wasikilizaji. Mikakati ya usemi katika nyimbo hudhihirisha nyenzo ambazo msanii ametumia kufanikisha maudhui yake. Tafiti mbalimbali zimedhibitisha kuwa lugha inayotumika katika nyimbo huonyesha taswira halisi ya maisha katika jamii. Picha halisi ya jamii hushamirishwa na fani mbalimbali za lugha. Kwa misingi hii mikakati ya usemi hudhihirisha masuala yanayokumba jamii wakati fulani. Sehemu hii inajadili tafiti za awali ambazo zimeangazia suala la nyimbo na mtindo ili kubainisha mwanya uliopo ambao Makala haya yanakusudia kuuziba.

Vipengele mbalimbali vya mtindo hutumiwa kukuza maudhui ya kazi husika. Hii huonyesha uhusiano wa karibu uliopo kati ya mtindo na maudhui. Nyandiwa (2015) aliangazia vipengele mbalimbali vya kimtindo vinavyoendeleza maudhui. Alichanganua baadhi ya vipengele vya lugha kama vile tashhisi, chuku, sitiari na kejeli katika tamthilia. Utafiti wake ulijaribu kuonyesha jinsi vipengele hivi vinavyoendeleza maudhui. Japo utafiti wake ulishughulikia vipengele vya kimtindo katika tamthilia na jinsi vinavyoendeleza maudhui, utafiti wake ulitufaa sana katika kuonyesha jinsi mikakati ya usemi iliyotumika katika Muziki inavyodhihirisha maudhui ya uanaharakati wa kijamii.

Mtindo hutumiwa kuwasilisha ujumbe wa msanii kwa namna ambayo huifanya hadhira kushawishika na kuamini yaliyomo. Chepkorir (2016) alichanganua mitindo katika tahariri ya gazeti la Taifa Leo. Katika utafiti wake aligundua kwamba tamathali za usemi na mbinu zingine zimetumiwa na mwandishi wa tahariri ya Taifa Leo. Alichunguza sitiari, misemo na tashbihi. Alipata kuwa sababu kuu ya kutumia tamathali hizi za usemi ni kujenga picha halisi ya hali ya mambo katika jamii kwa vile tahariri huzungumzia masuala yanayoathiri mwananchi wa kawaida. Uchunguzi wake ulionyesha kuwa mbinu hizi zimetumika kufanikisha kueleweka kwa ujumbe. Fauka ya kuwa utafiti wa Chepkorir ni tofauti na huu, ulikuwa tunu kwetu katika kuhakiki mikakati ya usemi iliyotumiwa kudhihirisha maudhui ya uanaharakati wa kijamii katika Muziki wa Genge.

Uhusiano wa karibu ulioko kati ya mtindo na maudhui ni mada ambayo imeshughulikiwa na wasomi wengi. Utafiti umeonyesha kwamba ni vigumu kutenga vipengele hivi ambavyo hujitokeza kama pande mbili za sarafu moja. Safinia (2017) alichunguza matumizi ya lugha katika tamthilia pamoja na dhamira zilizojitokeza ndani ya utumizi huo wa lugha. Alipata kuwa mwandishi ametumia vipengele tofauti vya lugha katika kuwasilisha maudhui kama vile tamathali za semi, lugha ya ishara, lugha ya picha, takriri, mdokezo, tanakali za sauti na nyinginezo. Aidha aligundua kuwa matumizi hayo ya lugha yaliibua maudhui tofauti kama vile kushajiisha ukombozi, kujenga umoja, kukemea usaliti, utabaka, umasikini, uongozi mbaya na kadhalika. Japo alijikita tu katika tamthilia, utafiti wake ulielekeza utafiti wetu katika kuhakiki jinsi mikakati ya usemi inavyotumika kuendeleza maudhui ya uanaharakati wa kijamii katika Muziki wa Genge.

Ojode (2017) alitafiti kuhusu kauli za istiari za taarab. Alipata kuwa nyimbo za taarab hujumuisha kauli za istiari katika kuwasilisha ujumbe. Kauli hizo za kistiari hutekeleza majukumu mbalimbali katika jamii yakiwemo kumulika mahusiano na changamoto zinazowakumba wanajamii. Utafiti wake ulidhihirisha kuwa kauli hizo huwa na manufaa kwa jamii husika kwani ni chombo cha kuangazia hali zinazokumba jamii. Ni jukwaa halisi la kushtakia dhuluma zinazoendelezwa katika jamii. Ingawa utafiti wake ni tofauti na huu kwani ulijikita katika nyimbo za taarab, ulitusaidia katika kuhakiki mikakati ya usemi inayodhihirisha uanaharakati wa kijamii katika Muziki wa Genge.

Utafiti wa Nkumbo (2019) ulichanganua matangazo ya ngono salama katika mtandao wa Durex Facebook Page Kenya. Utafiti huu ulichunguza mikakati ya kimawasiliano na mbinu za lugha katika matangazo ya Durex. Alipata kuwa mikakati ya usemi hufafanua jinsi maudhui au dhana fulani zinavyowasilishwa. Hata kama utafiti wake ulikuwa tofauti na huu ulitufaa sana katika kuhakiki mikakati ya usemi ambayo wasanii wa

Muziki wa Genge walitumia kudhihirisha maudhui ya uanaharakati wa kijamii. Utafiti wa Ndemo (2014) ulihusu uchanganuzi wa lugha ya amani na maridhiano katika muziki nchini Kenya. Ulilenga kuchanganua matumizi ya kipekee ya lugha na jinsi maudhui ya amani na maridhiano yanavyowasilishwa katika muziki. Utafiti huu ulichanganua upekee katika uteuzi wa maneno, vishazi na sentensi kwa kuzingatia uhusiano wa vipengele hivi kiwima na kimlalo. Utafiti huu ulibainisha kwamba kuna uteuzi wa kipekee wa lugha katika uwasilishaji wa ujumbe wa amani na maridhiano. Isitoshe, kupitia kwa utafiti huu ilibainika kwamba lugha huweza kutekeleza majukumu mbalimbali katika jamii. Majukumu haya ni kama vile: kuhimiza amani na maridhiano, kuionya jamii dhidi ya mienendo inayotishia amani na maridhiano pamoja na kutoa wasia wa jinsi ya kuhakikisha kwamba jamii inapata amani ya kudumu miongoni mwa majukumu mengine. Utafiti huu ulikuwa nguzo muhimu katika utafiti wetu katika kubainisha majukumu ya mikakati ya usemi iliyotumika katika Muziki wa Genge. Hata hivyo utafiti huu unatofautiana na wetu kwani umejikita katika maudhui ya Amani na maridhiano ilhali utafiti wetu umejikita katika maudhui ya uanaharakati wa kijamii.

Wambua (2012) alitafiti kuhusu mtindo na matumizi ya lugha katika nyimbo za Kakai Kilonzo. Alionyesha uhusiano kati ya uteuzi wa lugha na maudhui. Alielezea kuwa matumizi ya lugha katika kazi ya sanaa, hubainisha mitazamo mbalimbali ya wanajamii katika maisha yao. Katika utafiti wake aligundua kuwa wasanii wa muziki hutumia mbinu mbalimbali za lugha kuashiria matatizo yanayokumba jamii. Ingawa utafiti wake ulijikita katika nyimbo za Kakai Kilonzo, ulisukuma mbele utafiti wetu katika kuhakiki mikakati ya usemi iliyotumika kudhihirisha maudhui ya uanaharakati wa kijamii katika Muziki wa Genge.

Mikakati ya usemi ambayo imetumiwa na wasanii huwa na athari mbalimbali. Athari hizi zinaweza kuwa hasi au chanya. Huathiri kazi yenyewe inavyopokelewa na kufasiriwa na hadhira. Jumbe (2015) alitafiti kuhusu mikakati ya usemi katika muziki wa kizazi kipya. Katika utafiti wake alionyesha namna mikakati ya usemi inavyojitokeza katika nyimbo teule za muziki wa kizazi kipya. Aliangazia athari ya mikakati hii katika uhasi na uchanya wake. Utafiti wake ulidhihirisha kuwa athari hasi ni pamoja na vijana kujiingiza kwenye mahusiano ya kimapenzi katika umri mdogo na hivyo kuwa kwenye hatari ya kupata maradhi yakiwemo Ukimwi. Pia, aliona athari nyingine kuwa ni mmomonyoko wa maadili katika jamii kwa kuwa vijana hupenda kuigiza mambo yanayoimbwa katika tungo za wasanii husika. Pamoja na athari hasi, Jumbe alizungumzia athari chanya kama vile kuburudisha jamii, kudumisha mahusiano pamoja na kuwazindua wanajamii. Ingawa utafiti wake ulitofautiana na utafiti wetu, ulitufaa sana katika kuhakiki jinsi mikakati ya usemi katika Muziki wa Genge ilivyotumika kudhihirisha maudhui ya uanaharakati wa kijamii.

Utafiti wa Wandera-Simwa (2015) uliangazia fani za lugha katika hadithi za Abanyala (Mumbo) wa Kenya. Alielezea kuwa lugha ya usanii hujitokeza katika matumizi ya semi na tamathali mbalimbali. Aidha alifananua kuwa lugha hii ya usanii ndiyo hutofautisha kazi za sanaa na kazi nyingine kama vile za kijiografia, kisayansi na kihistoria. Pia alifafanua kuwa lugha hii hutekeleza majukumu mbalimbali. Utafiti wa Wandera-Simwa na wetu ni tofauti kwani yeye alichunguza hadithi ilhali utafiti huu ulichanganua nyimbo. Hata hivyo ulitufaa katika kuhakiki jukumu la mikakati ya usemi katika Muziki wa Genge ambapo utafiti huu ulijikita katika jukumu la kudhihirisha maudhui ya uanaharakati wa kijamii.

Ndung'u (2021) katika utafiti wake, alichunguza ulinganishi wa maumbo katika tendi za Mikidadi na Mayasa na Kalevala. Alichanganua vipengele vya kimaumbo katika tendi hizo na majukumu yake. Vipengele alivyoangazia ni pamoja na tashbihi, matumizi ya takriri, taswira, chuku, mbinu rejeshi, taashira, taharuki na sitiari. Aidha alitambua kuwa jukumu kuu la vipengele hivi katika tendi ni kumfikirisha msomaji zaidi na kumpa nafasi ya kujenga mawazo ili aweze kungámua ujumbe unaojitokeza. Licha ya kuwa Ndung'u alijikita katika tendi, utafiti wake uliufaa utafiti huu katika kudhihirisha jinsi mikakati ya usemi imetumika kuchochea hadhira kufikiria zaidi kuhusu matatizo yanayoikumba katika Muziki wa Genge.

**MATOKEO YA UTAFITI**

Kinachowasilishwa kama kauli ya usemi kinaweza kuhakikiwa kwa kuchunguza mikakati yake ya usemi. Kwa muktadha wa Makala haya mikakati ya usemi ni jumla ya tamathali za semi ambazo wasanii wa Muziki

wa Genge wametumia kuwasilisha maudhui ya uanaharakati wa kijamii. Aidha, maudhui yanaweza kuhakikiwa kwa mazingatio ya uwazi na usimbaji wa mikakati ya usemi ili kubaini viwango vya uanaharakati wa kijamii. Makala haya yalichunguza mikakati ya usemi ifuatayo: tashbihi, takriri, istiari, kinaya, maswali ya balagha na methali.

**Tashbihi**

Tashbihi ni mbinu ya uhamisho wa kimaana kwa kufananisha vitu ili kuchorea mtu picha akilini mwake kuhusu kitu kimoja kwa kukilinganisha na kingine kupitia matumizi ya maneno ya ulinganisho kama vile 'mfano wa', 'kama na 'mithili ya' (Hamad, 2017; Ndung'u, 2021). Mbinu hii ya tashbihi imetumiwa na wasanii wa Muziki wa Genge kudhihirisha maudhui ya uanaharakati wa kijamii. Kwanza kabisa mbinu hii inakuza picha mbalimbali akilini mwa hadhira ili kusawiri jinsi vijana wanavyohangaika kutokana na ukosefu wa ajira, ubaguzi, ufisadi pamoja na uongozi mbaya. Ufuatao ni mfano,

**Matini 1**

Wimbo **3 *Khalicartel 3*** Ubeti 4(15-16).

14. *But, pressure ya kuhomoka ndio imenikalia ka sofa* [lakini shinikizo la kutajirika limenikaza sana]
15. *Industry, ngori yaani ku manoeuvre si ni struggle* [taaluma umekuwa shida kwani yahitaji kupambana]
16. *Interviews, me siko booked, kama libu haina vitabu* [sijaitwa kwa mahojiano… ]

Wimbo**1 *Kuna siku Youth Wataungana*** Ubeti 3(5-8).

5. *Sina makao, ndio maana nimeishi kote*
6. *Ka Sila na Paul, milango ziliji-open* [kama vile kwa Sila na Paulo milango ilijifungua]
7. *Casino za tao, mipango zao ni all same* [mipango ya kamari za mjini zote inafanana]
8. *Nipate, nikose, nisote mpaka nikope*

Tashbihi zilizotumika katika matini hii zinadhihirisha maudhui ya ukosefu wa ajira. Katika Wimbo 3 msanii anadhihirisha vile vijana wana hamu ya kutaka kuishi maisha yenye ufanisi. Hata hivyo hawana uwezo huu kwani hawana kazi. Matini hii inadhihirisha jinsi vijana wamekumbwa na matatizo chungu nzima kutokana na ukosefu wa ajira. Tashbihi *kama libu haina vitabu* imetumiwa kutilia mkazo tatizo la ukosefu wa kazi. Japo vijana wamesoma hawapati nafasi za kazi; hata nafasi hizi zikitangazwa na wao wakaendelelea kutuma maombi, hawapati majibu yoyote. Wanajaribu kujinasua lakini wanashindwa licha ya kuwa na utashi wa kutaka kujitoa katika hali hii. Shauku kubwa ya kutaka kujinasua kutoka lindi la umaskini na kuwa tajiri (*kuhomoka)* ndiyo msanii anaelezea kuwa imemkalia kama sofa. Sofa ni aina ya kiti kikubwa na kizito. Hali hii inadhihirisha ugumu wa maisha ya vijana kwa kuwa hawana namna yoyote ya kujitoa kutoka hali hii ya umaskini. Tashbihi pia imetumika katika muziki wa Genge kukuza picha akilini mwa hadhira kuonyesha athari ya ukosefu wa kazi. Matini hii inakuza picha akilini mwa hadhira ambayo inabainisha matatizo yanayokumba vijana. Hawana makao bali wanaishi kurandaranda. Tashbihi *ka Sila na Paul, milango zilijiopen* imetumika kukuza picha akilini mwa hadhira kuonyesha jinsi vijana wanapata suluhu rahisi la matatatizo yao katika uchezaji kamari wakilenga kupata au kukosa. Wanaona kuwa hii ni fursa nzuri ya kupata pesa ilhali haya ni matendo maovu yasiyokubalika katika jamii.

**Takriri**

Takriri huhusu uradidi wa maneno katika mistari ili kuleta hisia fulani na kuteka nadhari ya hadhira. Kwa mujibu wa Senkoro (2011), takriri ni mbinu ya utunzi inayohusu urudiaji wa sauti, silabi, mistari, maneno na hata sentensi katika kazi ya fasihi kwa madhumuni maalum. Jilala (2016) anasema kuwa takriri ni mtindo wa usemi ambao msemaji hurudia neno au maneno yale yale kwa lengo la kutilia mkazo au kusisitiza jambo. Kulingana na utafiti huu takriri ni mkakati wa usemi ambao huhusu kusisitiza ujumbe kwa kurudia neno au kifungu cha maneno ili kuteka nadhari ya hadhira. Ni ujuzi wa kisanaa wa urudiaji wa maneno kimaksuudi katika matini. Msanii hulazimika kutumia takriri kwa kuamini kuwa akieleza jambo lake kwa kutumia neno moja tu halitaeleweka vizuri.

Takriri imetumika katika Muziki wa Genge ili kudhihirisha maudhui ya uanaharakati wa kijamii. Mbinu hii inatilia mkazo dhana mbalimbali za uanaharakati wa kijamii katika Muziki wa Genge. Dhana hizo ni pamoja na kuonya na kukashifu masuala ya ubaguzi, ufisadi na uongozi mbaya. Zaidi ya hayo imebainika kuwa mbinu hii imetumika kuhamasisha vijana wachukue hatua dhidi ya matatizo haya

yanayowakumba kama inavyojitokeza katika matini ifuatayo.

**Matini 2**

Wimbo **2 *Kwendaa*** Kibwagizo (1-8)

1. *Sipendi mangoma za Kenya (Kwenda! Kwenda!)*
2. *Mi sitambui Omollo (Kwenda! We kwenda!)*
3. *Ah, si huyu boy huringa? (Kwenda! Kwenda!)* [Ala! Huyu kijana huringa]
4. *Mi sijawahi hire madinga (Kwenda! Shenzi!)*
5. *Ah, mi sipendi hizo mangoma (Kwenda! Kwenda!)*
6. *Mi sitambui Omollo (Kwenda! Kwenda!)*
7. *Manze huyo boy huringa (Kwenda! We kwenda!)* [Aisee! Huyu kijana huringa]
8. *Mi sijawahi hire madinga (Kwenda! Shenzi!)* [Mimi sijawahi kukodi mashangingi]

Wimbo **4 *Tujiangalie*** Kibwagizo (1-9)

1. *Tujiangalie (Tujiangalie)*
2. *Tuko pabaya leo kuliko jana*
3. *Sikio la kufa halisikii dawa*
4. *Tuko kwa twitter tuna jibizana*
5. *Tujiangalie (Tujiangalie)*
6. *Tuko pabaya leo kuliko jana*
7. *Tusipo ziba ufa tuta jenga kuta*
8. *Tusake zetu*
9. *Tungali vijana*

Wimbo **1 *Kuna Siku Youth Wataungana*** Kibwagizo (1-7)

1. *Haina noma, huna namna*
2. *Tuseme "bora uhai," haina maana*
3. *Achia noma Maulana*
4. *Life kwenye streets kakiumana* [maisha mtaani hali ikiwa ngumu]
5. *Juu kuna siku youths wataungana* [ipo siku vijana wataungana]
6. *Kuna siku youths wataungana*
7. *Haina noma, huna namna*

Katika matini hii takriri imetumika kusisitiza ujumbe na kuteka nadhari ya hadhira. Kibwagizo cha Wimbo 2 kimerudiwa rudiwa ili kudhihirisha maudhui ya ubaguzi. Takriri ya neno *Kwendaa* imetumika kuwasuta wale wanaochukia nyimbo za wasanii wa Genge na kuhusudu nyimbo za wasanii wa kigeni. Zaidi ya hayo takriri hii imekusudiwa kuwakashifu wanaochukia wengine kwa msingi wa kabila lao. Msanii anawasuta wanaomchukia Omollo wakisingizia kuwa yeye huringa na hupenda maisha ya anasa ilhali ukweli ni kuwa Omollo anachukiwa kwa sababu ya kabila lake. Msanii anawazindua raia kujiepusha na kasumba za kikoloni na za kikabila. Isitoshe maneno *kwendaa* na *shenzi* yamerudiwarudiwa kote katika wimbo huu. Maneno haya yanerudiwa ili kukejeli raia ambao wanapendelea nyimbo za wasanii wa kigeni. Msanii anawasuta kwa kuwaita shenzi kwa maana kuwa ni wapumbavu na kuwataka wapotelee mbali kabisa. Msanii anaonyesha kuwa watu kama hawa ambao si wazalendo na wanaoendesha siasa za kikabila hawahitajiki katika jamii kwani wanarudisha nyuma taifa kimaendeleo.

Isitoshe, katika Wimbo 4 kuna uradidi wa neno *Tujiangalie*. Lengo hasa ni kuonya raia dhidi ya kuendelea kuukubali uongozi mbaya. Isitoshe, takriri hii imetumika kuwakemea na kuwatahadharisha viongozi kuwa wasipobadilisha mienendo yao ya ufisadi na uongozi mbaya, taifa litaporomoka. Aidha takriri ya silabi *tu* katika mistari hii yote ni njia ya kushajiisha raia ili wafahamu kuwa ni jukumu lao la kubadilisha hali ilivyo sawa na anavyosema Safinia (2017) kuwa mbinu ya uradidi hutumika kushajiisha hadhira ili waamke na wazinduke. Katika wimbo 1 takriri *Kuna Siku Youth Wataungana* imetumika kuwahamasisha vijana na kuwahimiza waungane. Msanii ametambua kuwa vijana wanakumbwa na matatizo mengi ndiposa anarudiarudia ujumbe huu wa kuungana pamoja kama suluhisho. Chambilecho Ndungú (2021), msanii ana weledi wa kurudiarudia maneno kimaksuudi ili kusisitiza ujumbe. Msanii anaamini kwamba ufanisi utapatikana tu baada ya muungano wa vijana ndiposa anasema *Wataungana (Wataungana, wafanye mambo)* ili kuwasilisha ujumbe huu kwa mkokotezo. Neno *mambo* limerudiwarudiwa ili kuwashajiisha vijana kuchukua hatua kama vile kuandamana ili kubadilisha hali ilivyo. Hivyo basi, takriri imetumika katika matini hii kuendeleza maudhui ya umoja kama njia ya kusuluhisha matatizo ya kijamii.

**Istiari**

Ojode (2017) anaelezea kuwa istiari ni matumizi ya neno au fungu la maneno kwa njia fiche. Neno huweza kutumiwa kimawazo katika kutoa wasifu wa kitu au mtu fulani kwa kujaribu kuonyesha kuwa vyote vina sifa sawa. Ni kule kuhamisha maana kutoka dhana moja hadi nyingine. Ndung'u (2021) anadai kuwa kinachohamishwa ni tabia, umbo, au kazi ya kitu kwa kuihusisha na tabia au kazi ya kitu kingine. Hali hii

hutokea tu iwapo msemaji wa kauli ana uwezo wa kulinganisha mambo tofauti katika mazingira yake. Fasiri hii inalandana na uchunguzi wetu kwa kuwa wasanii wa Muziki wa Genge kwa kiwango fulani wametumia kauli zenye istiari kuchochea fikra za hadhira. Istiari hizi zimetumika kuendeleza maudhui ya uanaharakati wa kijamii katika Muziki wa Genge kama inavyojitokeza katika matini ifuatayo.

**Matini 3**

Wimbo **3 *Khalicartel 3*** Ubeti 7 (3-5):

3. *Najua ni nyinyi bado hukaa kwa hizo keja zina parking* [Najua ni nyinyi bado hukaa kwa nyumba zenye maegesho]
4. *Bado bado ndani ya ofisi mmejaza ma vitambi*
5. *Na raundi hii kukuwa fisi ngumu juu wanafuata maganji* [na awamu hii kushiriki uasherati si rahisi kwa kuwa wanazingatia pesa]

Ubeti 9 (4-8)

4. *Kwanza kabla mambo yote wacha kwanza nishukuru*
5. *Hii nafasi nimepata ya kuweka akili huru*
6. *Dunia haina haki, ni shamba la wanyama*
7. *Wale wachache tumebaki mashida zinatuandama*
8. *Sina rent, sina dishi, kila siku jo na struggle* [kwa sababu ninajaribu kujichumia na kukwepa matata]

Ubeti 9 (10-12)

10. *Kukaa bila janta inaweza fanya msee adedi* [kuishi bila pesa kunaweza kumfanya mtu kufa]
11. *Ndio me hujam nikiwacheki, matapeli ma poacher* [ndio sababu ninakerwa kuwaona matapeli na majangili]
12. *Wanataka kunyonya maskini nirudi ocha* [wanataka kuwalaghai maskini warudi mashambani]

Istiari zinazojitokeza hapa zimetumika kuchochea hadhira kufikiria zaidi kuhusu yanayotendeka katika jamii. Istiari ya *kuweka akili huru* inadhihirisha jinsi msanii amefurahi kupata nafasi ya kuangazia matatizo ambayo vijana wanapata katika jamii. Kuweka akili huru ni istiari inayoonyesha kuwa yeye haogopi na ataelezea kinagaubaga yanayotendeka katika jamii. Istiari *dunia ni shamba la wanyama* inaonyesha ukosefu wa haki na usawa ambapo kuna wanaonufaika na wengine wanaangamia katika lindi la umaskini.

Aidha, utafiti huu umebainisha kuwa mbinu hii ya istiari imetumika kudhihirisha uongozi mbaya fauka ya kubainisha changamoto zinazowakumba vijana. Istiari za *vitambi, parking, matapeli na mapoacher* zimetumika kudhihirisha uongozi mbaya ambao umewasababishia vijana matatizo chungu nzima. Kitambi huashiria ulafi mwingi walio nao viongozi. Wanawanyima vijana nafasi za kazi kwa kukatalia ofisini na kuendelea kuwapa ahadi za uongo. Isitoshe mbinu hii imetumika kujenga picha akilini mwa hadhira na kuchochea hadhira ifikirie zaidi kuhusu masuala haya yanayowakumba vijana. Hatimaye hadhira itazinduka kisha itaanza kufanya maamuzi ya busara.

**Kinaya**

Kinaya ni tamathali ya usemi inayohusisha ukinzani kati ya hali ilivyo na inavyosemekana kuwa (Chimerah & Njogu, 1999). Ni kauli ambayo ina maana ya kinyume cha matarajio au matumaini (Msokile, 1993). Dhima ya kinaya ni kuibua ujumbe kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa kukejeli au kwa kutia chuku kwa lengo la kusisitiza. Wasanii wa Muziki wa Genge wametumia kinaya kukejeli uongozi mbaya pamoja na unafiki wa viongozi kama inavyojitokeza katika matini ifuatayo.

**Matini 4**

Wimbo **5 *Wajinga Nyinyi*** Ubeti 2 (2-10)

2. *Si mnajua nyinyi voters ndio washenzi?* [si mnajua nyinyi wapiga kura ndio washenzi]
3. *Kwani hamjui mdomo yangu ilibatizwa na wakongwe?*
4. *So nashanga akili zenu time ya kura zinajaanga shonde?*
5. *Na hiyo wiki ndo najua jirani yangu huwa Mjaka*
6. *Kamah kumbe huwanga msapere* [kumbe Kamau huwa Mkikuyu]
7. *Ata salamu hatapata*
8. *Piga tu kura na utalala bila kula, a night of tears* [Piga tu kura na utalala ukilia kwa kukosa chakula]
9. *Nani skiza na macho na ona with your ears* [sikiliza kwa macho na uone kwa masikio]

Wimbo **4 *Tujiangalie*** Ubeti 6 (3-6):

3. *Ku admire mwizi amemake it* [kushangilia ufanisi wa mwizi]
4. *Story za shamba wamegrab* [visa vya kunyakua mashamba]
5. *Mkono nahonga imevaa*

6. *Bracelet ya colors za flag* [bangili yenye rangi ya bendera]

Katika Wimbo 5 mbinu ya kinaya imetumika kuwakemea raia kwa kuongozwa na ukabila wakati wa kupiga kura. Msanii anawashtumu kuwa wakati wa kupiga kura ndio wao hutambua makabila ya majirani zao. Katika mstari 7 anasema *Kamah kumbe huwanga msapere*. Aidha, anawasuta raia kwa kutofanya uamuzi wa busara wakati wa uchaguzi jambo ambalo linawaathiri na kuwaletea majuto baadaye kama anavyoeleza katika mstari 9, *Piga tu kura na utalala bila kula, a night of tears*. Kinaya kimetumika kuwazindua raia wachague viongozi wanaofaa ili kuepuka madhara ya uongozi mbaya. Mbinu hii ya kinaya pia imetumika katika Wimbo 4. Kinaya kimetumika kuwashambulia raia ambao husifu viongozi fisadi ambao wamejilimbikizia mali ya umma. Hili linajitokeza katika mistari 3-4, *Ku admire mwizi amemake it … Story za shamba wamegrab.* Aidha kinaya kimetumiwa kuwasuta viongozi fisadi ambao hujifanya wazalendo kwa kuvaa bangili zenye rangi ya taifa. Msanii anawazindua raia kwa kuwatahadharisha dhidi ya viongozi kama hawa.

**Maswali ya Balagha**

Maswali ya balagha ni mbinu ambayo hutumiwa kutanabahisha hadhira kwa kuuliza maswali bila kutarajia majibu. Haya ni maswali ambayo huwa ni maneno ya kuchoma, kukata na kutia uchungu kwa lengo la kuhamasisha (Nyandiwa, 2015). Maswali ya balagha ni mbinu nzuri ya kuifikirisha hadhira, kuishawishi kuhusu jambo au hali fulani; na pia kusisitiza usemi (Chepkorir, 2016). Maswali ya balagha katika Muziki wa Genge yanatekeleza majukumu maluum. Kwanza kabisa dhima ya maswali ya balagha ni kutoa mawazo au hisi za ndani za msanii au kuweka jambo fulani wazi kwa hadhira na ambalo linahitaji kuangaziwa kwa makini. Aidha, maswali ya balagha yanatumiwa kusisitiza wazo ambalo msanii hakudhamiria kulieleza tu bali kulitaja bayana. Mbinu hii imetumika katika matini ifuatayo.

**Matini 5**

Wimbo **5 *Wajinga Nyinyi*** Ubeti 2 (2-10)

*2022 already, si mnajua nani ni Prezzi?* [tayari 2022 si mnajua nani ni rais]
*Si mnajua nyinyi voters ndio washenzi?* [si mnajua nyinyi wapigakura ndio washenzi]
*Kwani hamjui mdomo yangu ilibatizwa na wakongwe?*
*So nashanga akili zenu time ya kura zinajaanga shonde?*
*Na hiyo wiki ndo najua jirani yangu huwa Mjaka*

Maswali ya balagha yanayojitokeza hapa yanakusudiwa kuweka wazi swala la upigaji kura. Maswali haya yanalenga kuwapiga ndaro raia wanaozubaa wakati wa kupiga kura. Maneno kama *shenzi* na *shonde* yanachoma na kuudhi. Shenzi lina maana ya mjinga au mpumbavu ilhali shonde ni kisawe cha mavi hasa ya binadamu. Hata hivyo, maneno haya yametumika kushtumu raia ambao wanakosa kufanya uamuzi wa busara wakati wa uchaguzi. Wao huishia kuwachagua viongozi waovu ambao wakichukua madaraka hukengeuka na kuwa manyang'au, mafisadi, mafedhuli, wenye tamaa za madaraka na ujasiri wa kulikandamiza tabaka la wanyonge. Msanii ametumia maswali haya ya balagha kwa lengo la kuhamasisha na kufikirisha hadhira kwa kutumia maneno yenye mchomo wa hisia pale wanaishia kujiuliza mbona wanahusishwa na ushenzi na shonde. Mtindo huu wa maswali ya balagha umetawala wimbo huu ili kuifikirisha hadhira na kuitaka ibadili hali hii inapotafuta majibu ya maswali haya.

**Methali**

Kulingana na Kuvuna (2013), methali ni kauli fupi inayosheheni maana na ujumbe na inayochukuliwa na jamii kuwa kiwakilishi cha hekima na busara. Methali imefafanuliwa na Wamitila (2001) kuwa ni msemo ambao unajitosheleza, ulio na maana nzito, muundo wa kishairi, ambao unadhamiriwa kuadibu au kuelekeza, kushauri na kadhalika. Hivyo basi, methali hufafanua maudhui kupitia maana na ujumbe uliomo. Hubeba maana pana kuliko maneno yanayotumiwa katika methali husika. Kwa mujibu wa utafiti huu ni bayana kuwa methali zimetumika kukejeli, kuonya, kushauri pamoja na kuhamasisha jamii kuhusu ufisadi pamoja na uongozi mbaya jinsi inavyojitokeza katika matini ifuatayo.

**Matini 6**

Wimbo **4 *Tujiangalie*** Kibwagizo (1-9)

1. *Tujiangalie (Tujiangalie)*
2. *Tuko pabaya leo kuliko jana*
3. *Sikio la kufa halisikii dawa*
4. *Tuko kwa twitter tuna jibizana*

5. *Tujiangalie (Tujiangalie)*
6. *Tuko pabaya leo kuliko jana*
7. *Tusipo ziba ufa tuta jenga kuta*
8. *Tusake zetu*
9. *Tungali vijana*

Methali *sikio la kufa halisikii dawa* na *tusipoziba ufa tutajenga kuta* zimetumika ili kuonya na kuhamasisha raia dhidi ya uongozi mbaya. Msanii anaeleza kuwa raia pamoja na viongozi wanapaswa kuwajibika katika ujenzi wa taifa. Raia waajibike katika kuchagua viongozi wanaofaa nao viongozi waajibike katika uongozi wao. Aidha, msanii anaonya kuwa hili lisipotendeka taifa litaporomoka au kurudi nyuma kimaendeleo. Hatimaye watalazimika kujenga *kuta* kumaanisha kuwa itakuwa kibarua kigumu kulifanya taifa lisonge mbele.

**MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

**Mahitimisho:** Makala haya yametambulisha mikakati ya usemi iliyotumika kudhihirisha maudhui ya uanaharakati wa kijamii katika Muziki wa Genge. Nyimbo hupimwa uzuri wake kwa kuzingatia mikakati inayotumika kupitisha ujumbe kwa hadhira. Mtafiti amepata kuwa picha ya hali halisi ya maisha ya vijana imedhihirishwa kupitia kwa mikakati ya usemi iliyotumiwa na wasanii wa Muziki wa Genge. Wasanii hawa wamedhihirisha matatizo yanayowakumba vijana. Zaidi ya hayo wametumia tashibihi, takriri, methali, istiari balagha na kinaya ili kuzindua vijana na kuwahamasisha wachukue hatua zitakazowanufaisha maishani Kwa kutumia nadharia ya Uchanganuzi hakiki wa usemi katika kuchambua mtindo wa usemi katika Muziki wa Genge tumethibitisha mambo kadhaa. Kwanza, tumeona kuwa mikakati ya usemi ni nyenzo muhimu aliyo nayo msanii ya kumwezesha kujieleza ili kuathiri hadhira yake kwa namna anayoikusudia. Kadhalika, mikakati ya usemi ni ala ya kuwasilishia maudhui. Hatimaye, Makala haya yamebainisha wazi kuwa wasanii wa Muziki wa Genge wamefanikiwa kudhihirisha maudhui ya uanaharakati wa kijamii katika muziki huu. Muziki huu basi umekuwa nyenzo maarufu ya kuendeleza uanaharakati wa kijamii.

**Mapendekezo:** Kwa mujibu wa makala haya ni wazi kuwa Muziki wa Genge ni jambo lisiloweza kupuuzwa kwani ni jukwaa la vijana la kuendeleza uanaharakati wa kijamii. Ni mapendekezo yangu kuwa tafiti za baadaye zinaweza kushughulikia sehemu zifuatazo:Utafiti linganishi kuhusu aina ya Muziki wa Genge na aina nyingine ya muziki kama vile taarabu au zilizopendwa, utafiti kuhusu kuchanganua mtindo mingine na fani inayotumika katika Muziki wa Genge, utafiti kuhusu maudhui mengine yanayojitokeza katika muziki wa Genge, kwani mtafiti alijikita tu katika maudhui ya uanaharakati wa kijamii, utafiti kuhusu matumizi ya misimu katika Muziki wa Genge na utafiti kuhusu istiari dhana zinazotumika katika Muziki wa Genge.

**MAREJELEO**


Chepkorir, F. (2016). *Uchanganuzi wa mtindo katika tahariri ya gazeti la Taifa Leo* (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Finnegan, R. (1970). *Oral literature in Africa*. Oxford University Press.

Hamad, M. A. (2017). *Muundo wa lugha katika mashairi ya watungaji wateule wa Zanzibar* (Unpublished doctoral dissertation). State University of Zanzibar.

Jilala, H. (2016). *Misingi ya fasihi linganishi: Nadharia, mbinu na matumizi*. Daud Publishing Company.

Jumbe, A. (2015). *Matumizi ya lugha katika muziki wa kizazi kipya: Mifano kutoka katika nyimbo za mapenzi za wasanii Inspecta Haroun na Mwanafalsafa* (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Kidula, N. (2012). The local and global in Kenyan rap and hip-hop culture. In E. S. Charry (Ed.), *Hip hop Africa: New African music in a globalizing world* (pp. 171–186). Indiana University Press.

Kiongera, K. (2010). *Mchango wa vijana katika mabadiliko chanya katika tamthilia nne za Kiswahili* (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kenya National Bureau of Statistics. (2022). *Economic survey*. Government Printer.

Koster, M. M. (2013). The hip hop revolution in Kenya: Ukoo Flani Mau Mau, youth politics and memory, 1990–2012. *The Journal of Pan African Studies, 6*(3), 82–105.

Leech, G. (1969). *Style in fiction: An introduction to English fictional prose*. Longman.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya uhakiki wa fasihi*. East African Educational Publishers.
Ndemo, P. M. (2014). *Uchanganuzi wa lugha ya amani na maridhiano katika muziki nchini Kenya (2008–2012)* (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Moi.
Ndung'u, J. N. (2021a). *Ulinganishi wa maumbo, motifu na changamoto za majagina katika tendi za Mikidadi na Mayasa na Kalevala* (Tasnifu ya uzamifu ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Laikipia.
Ndung'u, J. N. (2021b). *Ulinganishi wa maumbo na motifu katika tendi za Mikidadi na Mayasa na Kalevala* (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Laikipia.
Ngugi, M. (2000). Nafasi ya muziki uliopendwa katika fasihi ya Kiswahili. *Swahili Forum, 7*, 145–152.
Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation.
Nkumbo, D. (2019). *Uchanganuzi wa matangazo ya ngono salama katika mtandao wa Durex Facebook page Kenya* (Tasnifu ya uzamifu ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Laikipia.
Ntarangwi, M. (2009). *East African hip hop: Youth culture and globalization*. University of Illinois Press.
Nyandiwa, H. (2015). *Uchanganuzi wa kimtindo wa Zinguo na Mbaya Wetu* (Unpublished master's thesis). University of Nairobi.
Ojode, J. O. (2017). *Uchanganuzi kipragmatiki wa sitiari katika nyimbo za taarab: Mfano wa Mzee Yusuf na Mwanahawa Ally, Unguja* (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kisii.
Safinia, K. A. (2017). *Kuchunguza matumizi ya lugha na dhamira katika tamthilia teule za mwandishi Emmanuel Mbogo* (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Tanzania.
Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi: Mfululizo wa lugha ya fasihi*. KAUTTU.
The Republic of Kenya. (2010). *The Constitution of Kenya*. Government Printer.
Wambua, S. M. (2012). *Mtindo wa nyimbo za Kakai Kilonzo* (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
Wamitila, K. (2001). *Kamusi ya methali*. Longhorn Publishers.
Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya fasihi: Istilahi na nadharia*. Focus Publications.
Wandera-Simwa, S. P. (2015). *Taswira za kimenke katika hadithi za Abanyala (Mumbo) wa Kenya* (Tasnifu ya uzamifu ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Laikipia.
Wasike, C. (2011). Jua Cali, genge rap music and the anxieties of living in the glocalized city of Nairobi. *Muziki: Journal of Music Research in Africa, 8*(1), 18–33. https://doi.org/10.1080/18125980.2011.570073